JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Barabara ya Bombo Hospitali,
S.L.P 1953,
21105 TANGA,
Simu Nambari: (027) 2645186
Nukushi: (027) 2647885
Barua Pepe: rbctangal@pccb.go.tz
Tovuti: www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

MEI 28, 2020

TAKUKURU MKOA WA TANGA YAINGILIA KATI MALALAMIKO YA WAZAZI DHIDI YA UONGOZI WA SHULE YA SEKONDARI ST. MARY'S MAZINDE JUU

Ndugu wanahabari,

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweka salama na kutukutanisha tena siku ya leo kwa ajili ya kutoa taarifa fupi kuhusu TAKUKURU ilivyoweza kuingilia kati malalamiko ya baadhi ya wazazi na walezi wenye watoto wanaosoma shule ya Sekondari ya ST. MARY'S MAZINDE JUU.

Ndugu wanahabari,

Mnamo tarehe 25/05/2020 Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa TANGA ilipokea malalamiko kutoka kwa baadhi ya wazazi na walezi wenye watoto wanaosoma kidato cha sita katika Shule ya Sekondari ST. MARY'S MAZINDE JUU iliyoko Wilaya ya Lushoto Mkoani Tanga kwamba wamepewa maagizo kupitia kundi la wazazi la WhatsApp kwamba wanatakiwa kulipa fedha za ziada kabla ya kuwarudisha shule watoto wao ambao ni wanafunzi wa kidato cha sita.

Malalamiko ya wazazi hao yalikuwa yakimtuhumu Mkuu wa shule hiyo kuwa amewataka wazazi na walezi wa wanafunzi wa kidato cha sita kulipa kiasi cha Shilingi 750,000/= (shilingi laki saba hamsini elfu tu) kwa kila mmoja kabla ya tarehe 01/06/2020.

Malalamiko hayo yalieleza kuwa fedha hizo ni malipo ya ziada kwa kila mwanafunzi wa kidato cha sita kwa ajili ya kuwalipa waalimu na wafanyakazi wengine katika kipindi ambacho wanafunzi hao watakuwa shuleni hapo kujiandaa na mitihani yao ya kuhitimu kidato cha sita.

Jambo hilo la kutoa malipo ya ziada lilionekana kuwakera wazazi na walezi wenye wanafunzi wa kidato cha sita shuleni hapo kwa sababu walieleza kuwa walikuwa wameshalipa ada inayotakiwa kabla ya kufungwa shule baada ya kuibuka janga la ugonjwa wa korona na kimsingi hawakutakiwa kudaiwa malipo ya ziada.

Aidha wamelalamika kuwa walikuwa wameshalipa Shilingi laki moja kwa kila mwanafunzi ili wabakie shuleni kujiandaa na masomo wakati wa likizo na kwamba hawakubaki shule kutokana na kuibuka maradhi ya corona (COVID 19) ambapo wote walirudishwa nyumbani kwa maelekezo ya Serikali na hawajui fedha hiyo imefanyia nini.

Ndugu wanahabari,

Baada ya kupata malalamiko hayo ya baadhi ya wazazi na walezi TAKUKURU Mkoa wa Tanga kupitia kwa Mkuu wa TAKUKURU Wilaya ya Lushoto ilifanya ufatiliaji kwa lengo la kupata ukweli wa tuhuma hizo.

Uchunguzi wa TAKUKURU ulifanyika kwa kuwasiliana na uongozi wa shule hiyo ambapo umeweza kuthibitisha kuwa tuhuma hizo ni za kweli na kwamba wazazi na walezi wa wanafunzi 178 kati ya 222 wa kidato cha sita, walitakiwa kulipa kiasi hicho cha fedha yaani shilingi 750,000/- kabla ya kufunguliwa shule tarehe 01/06/2020. Wanafunzi wengine 44 wanasoma shuleni hapo kwa ufadhili wa shule na wafadhili mbalimbali na hivyo tangazo hilo lilikuwa haliwahusu.

Kwa maana hiyo jumla ya Shilingi 133,500,000/- zilitarajiwa kukusanywa na shule kutokana na malipo hayo ya ziada na hadi kufikia tarehe 27/05/2020 tayari wanafunzi wanne walikuwa wameshalipiwa na wazazi au walezi wao jumla ya Shilingi 3,000,000/= kupitia akaunti ya shule.

Ndugu Wanahabari,

Uongozi wa shule hiyo ulipohojiwa na TAKUKURU Wilaya ya Lushoto tarehe 27/05/2020 kwa lengo la kutoa ufafanuzi juu ya tuhuma hizo, katika maelezo yake Mkuu wa shule alieleza kuwa wazo la malipo hayo ya ziada lilitokana na wazazi wenyewe kwenye kundi lao la WhatsApp na kwamba yeye alikubaliana nao baada ya kuona ni wazo jema.

Hata hivyo, baada ya kuona mjadala wa wazazi katika kundi hilo unakuwa mkali aliwaeleza kuwa malipo hayo siyo lazima bali atakayependa alipe na anayeona hawezi asilipe.

Ndugu Wanahabari,

Baada ya kuchambua maelezo ya mkuu wa shule na ushahidi uliopatikana, TAKUKURU na uongozi wa Shule ya Sekondari ya ST. MARY’S MAZINDE JUU walikubaliana yafuatayo yafanyike ili kuondoa malalamiko hayo:

(i) Mkuu wa shule aandike waraka wa kufuta mjadala huo wa malipo ya ziada ya Shilingi 750,000/= akiwaeleza wazazi kuwa hawatakiwi kulipa fedha hizo.

(ii) Wazazi wajulishwe uamuzi huo wa shule kupitia makundi ya WhatsApp ambayo yalitumika kutoa taarifa ya malipo hayo ya ziada.

(iii) Wazazi wote waliokwisha lipa kiasi hicho cha fedha warejeshewe.

Maagizo mawili ya mwanzo yameshatekelezwa na agizo la tatu linaendelea kutekelezwa.

Ndugu wanahabari,

Napenda pia kutoa wito na kuwakaribisha wananchi na wadau wote wa Mapambano Dhidi ya Rushwa kufika katika ofisi zetu kutoa taarifa kwa njia yoyote watakayoona muafaka kwao.

Mwananchi au mdau yeyote anaweza kuwasiliana moja kwa moja na ofisi za TAKUKURU Mkoa wa Tanga kwa ajili ya kutoa kero au malalamiko yake na tunaahidi yatafanyiwa kazi. Pia mtoa taarifa anaweza kupiga simu ya Bure 113 au ukatuma ujumbe mfupi wa maandishi kwa kupiga *113# na kufuata maelekezo.

ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA

Imetolewa na:

DKT. SHARIFA BUNGALA

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa TANGA